

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI



ANGALIENI ATHARI ZA MIKOPO ZINAZOWEZA KUHATARISHA UCHUMI

Hayo yamesemwa Bw. Viñals José ambaye ni Mkurugenzi wa Idara ya Fedha na Masoko ya Mitaji alipokuwa akiongea na waandishi wa habari mjini Washington DC.

Bw. José alieleza kuwa tunaona kuwa katika ripoti yetu hii hatari ya kuyumba kwa uchumi imeondoka. Sera imara zimeweka uchumi kuwa imara na madhubuti zaidi ya tulivyotegemea. Soko la Dunia limekuwa na uchumi umerudia katika hali yake ya kawaida. Hii imesaidia kuondoa viashiria vya hatari na vilevile imesaidia Taasisi zetu za fedha kuwa makini.

Pamoja na kuwa uchumi umeimarika bado kuna mambo muhimu ambayo tunapaswa kuyazingatia kama vile hatari zinazoweza kujitokeza hasa kwenye madeni na kuhakikisha kunakuwa na uangalifu wa hali ya juu na kuyafuatilia.

"Tukiangalia kwenye mifumo ya mabenki, inatia moyo kwani uchumi umeimarika na soko la fedha limeongezeka. Makadirio ya kushuka kwa mabenki yameongezeka kwa \$500 billion, kutoka \$2.8 trillion mpaka \$2.3 trillion, na makadirio ya mbili ya tatu yamegundulika hadi sasa. Zaidi ya hapo uwiano wa mitaji ya mabenki kwa ulaya na Marekani umeimarika, na mabenki yameongeza mitaji na kufurahia pato la muda lililoongezwa". alisisitiza mchumi huyo.

Pamoja na mafanikio haya, mabenki bado yanatakiwa kuwa na mitaji mikubwa ukizingatia kuwa hiyo iliyonayo ni ile ambayo imepatiwa na shirika la fedha la kimataifa, hivyo basi hawana budi kujifunga mkanda na kutoridhika kuwa sasa wana mitaji ya kutosha. Kwa maana hiyo mabenki yote yajue kuwa yana changamoto kubwa ya kifedha ambayo ni kama takriban \$5 trillion hadi kufikia miaka mitatu ijayo.

Aliongeza kuwa pamoja na matokeo hayo, mifumo ya mabenki itatakiwa kuwa na msukomo mkubwa wa kuhakikisha kuwa mikopo yote inalipwa japo itakuwa kidogo kidogo na kwa muda. Pia kuwepo kwa uwezo wa kukopesha japo itaendelea kuwa dhaifu. Mikopo ya kuweka dhamana itakuwa na riba kubwa na kutakuwa na ukopeshaji mdogo kwa asasi binafsi hadi hapo mambo yatakapokuwa mazuri kabisa.

Nikiangalia katika athari za uwekaji dhamana kwa kukopeshwa. Ongezeko la deni la Taifa na hatari ya kunyang'anywa dhamana ni changamoto kubwa inayotukabilialiongeza Bw. José.

Aidha alisema kuwa ningependa kuzungumzia ujumbe muhimu kuhusu sera na kueleza kuwa wao kama wachumi wana sera nne.

Kwanza ni uangalifu katika mikopo ambayo inaweza ikahatarisha uchumi wa dunia sio tu kwa mambo ya fedha za umma bali pia kwa uimara wa fedha zote. Watunga sera ni lazima waendeleze na wawasiliane katika kupanga mambo ya fedha ili kuondoa matatizo yanayoweza kuathiri mambo ya mtiririko wa fedha.

Pili ni kuhakikisha kuwa kunautendaji ambao utatufikisha salama, kiushindani na katika mfumo wa fedha ambao ni rahisi kuuweka tunavyohitaji. Mabenki lazima yapitie upya taratibu zao zote za utoaji wa mikopo na kuwa makini kwa wanaowapa mikopo hiyo.

Tatu, ni upatikanaji wa mikopo. Watunga sera kutoka katika nchi zile zinazopata mitaji mikubwa wanatakiwa kuwa na sera imara ambazo zitalinda soko la fedha na si kuachia mzunguko wa fedha uende wenyewe.

Mwisho, ujumbe wetu ni kwamba tunahitaji kuweka sera imara ambazo zina msingi imara kiusalama, kiushindani, na kimfumo wa kifedha ambao unaweza kubadilishwa kwa haraka. Tunatakiwa kuwa makini na ni muhimu kufanana katika sera kimataifa. Alisisitiza José.

Pamoja na kuwa na unafuu katika hali ya fedha bado tunatakiwa kuwa makini sana, tusijisahau na tukafikiri kuwa uchumi hauwezi kutetereka. Hivy tunachopaswa kufanya ni kuziba mianya yote ile ambayo tumeigundua. Huu sasa ni wakati wa kuhakikisha kuwa uchumi hauyumbi na ni wakati wa kuzitangaza sera muhimu na kuleta mabadiliko.

Haya ni baadhi ya mambo muhimu yaliyojadiliwa katika ripoti inayohusu mambo ya Fedha na Uchumi.

**TAARIFA HII IMETOLEWA NA MSEMAJI MKUU
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI
WASHINGTON DC
21/4/2010**